

Dkt. Nchemba ahimiza ufugaji wa kisasa kuisisimua uchumi na maisha ya watu

NA BENNY MWAIPAJA,
DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ameishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kusimamia kikamilifu sekta ya mifugo kwa kubuni njia mbalimbali zitakazoongeza tija katika sekta hiyo.

Dkt. Nchemba alitoa ushauri huo Jijini Dodoma, alipokutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa Wizara hiyo pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, kujadili masuala mbalimbali yanayohusu namna ya kuboresha sekta ya mifugo ili iweze kuongeza mchango katika ukuaji wa uchumi wa nchi na maendeleo ya watu.

"Tutakavyo weka mipango ya kisasa ya kukuza uzalishaji katika eneo hili la mifugo, tutatengeza wigo mkubwa wa walipakodi, tutabadilisha maisha ya watu wetu, tutakuza uchumi na ajira" alisema Dkt. Nchemba

Alisema kuwa maende-

leo ya sekta ya viwanda yanayokwenda kwa kasi hapa nchini yanahitaji malighafi za kulisha viwanda hivyo na kwamba fursa zilizopo kwenye sekta ya mifugo ni kubwa na kushauri mbinu za kisasa za kuendeleza ufugaji ziwekwe bayana na kufanyiwa kazi ipasavyo.

Alisema utaratibu wa sasa wa wafugaji kuhamahama na mifugo kwa ajili ya kutafuta malisho na maji umepitwa na wakati na kuahidi kuwa Wizara yake iko tayari kutoa ushirikiano ili kufanikisha mipango ya kuendeleza sekta ya mifugo nchini.

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Ndaki, alimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kukutana na vingozi wa Wizara hizo mbili na kuahidi kuwa ushauri ulitolewa utafanyiwa kazi kikamilifu ambapo ameunda timu ya wataalamu kwa ajili ya kuchambua mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa katika kikao hicho alichosema

kilikuwa ni cha muhimu.

"Tutaangalia namna ya kupanua na kuwa na maeneo maalum ya malisho ya mifugo yetu pamoja na kuboresha ufugaji ili ubadilike kutoka ufugaji wa kiasili kwenda ufugaji wa kisasa ili kuongeza tija" alifafanua Mhe. Ndaki

Alisema kuwa wafugaji watakaokuwa tayari kubadilisha namna ya ufugaji wao watapelekwa kwenye maeneo hayo yatakayowekewa miundombinu yote muhimu ya ufugaji ikiwemo maji, majani ya malisho na maji.

Wakizungumza katika kikao hicho, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Emmanuel Tutuba, aliishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuanzisha maeneo ya ufugaji (Runch) kila mkoa na kujenga miundombinu itakayowasaidia wafugaji kufuga mifugo yao kisasa ili waweze kuongeza kipato chao, kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi na kuondokana na umasikini.

P
ki

NA
OR

KA
Ta
za
do
wa
za
Se
m
ki

sh
P
ta
fi
k
r
r

Tanzania uk. 4, 7/05/2021

Ukurua, 7/05/2021

Wizara yawataka wafugaji kuacha kufuga kimazoea

MOROGORO NA WARIOBA IGOMBE

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imewataka wafugaji nchini kuachana na ufugaji wa mazoea na badala yake kuwa na ufugaji wenye tija na endelevu ili kukuza uchumi wa nchi.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani Dk. Angello Mwilawa.

Lengo la serikali ni kuendeleza jitihada zilizopo ili kuhakikisha tunafikia malengo ya kuwafanya wafugaji wote kuondokana na ufugaji wa kimazoea na kufuga ufugaji wenye tija kwa lengo la kuongeza thamani alisema Mwilawa.



Lengo la serikali ni kuendeleza jitihada zilizopo ili kuhakikisha tunafikia malengo ya kuwafanya wafugaji wote kuondokana na ufugaji wa kimazoea na kufuga ufugaji wenye tija kwa...

Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani Dk. Angello Mwilawa.

Dk. Mwilawa alisema lengo ni kutoka kwenye ufugaji wa mazoea na kwenda kwenye ufugaji wenye tija na endelevu ili kukuza uchumi wa nchi na kuongeza mnyororo wa thamani kwa wakulima wanaojishughulisha na kazi za kifugaji.

Alisema kutokana na hilo wizara imekuwa ikitoa mafunzo kwa wananchi wa mikoa mbalimbali kwa lengo la kuwataka kuwa mabalozi wazuri katika suala la ufugaji wa kisasa ili kuweza kuongeza tija kwenye sekta hiyo.

Dk. Mwilawa alisema uboreshaji katika sekta ya mifugo nchini, kutasaidia kuongeza thamani ya mifugo na mazao yake yote hali itakayokuza uchumi wa wafugaji na pia pato la taifa litaongezeka.

Aidha, aliwapongeza wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo cha mkoani hapa kwa kuonyesha uzalendo kwa jamii.

Naye, Mkurugenzi wa Umoja wa Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Revocatus Kimario (SUGECO) alisema uongozi wa umoja huo umekuwa ukitoa mafunzo kwa wananchi juu ya kilimo, biashara na ufugaji.

Mkurugenzi huo alisema, lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wananchi hasa vijana kutoka mikoa mbalimbali nchini kuwa mabalozi wazuri katika kuelimisha wafugaji kujikita kwenye ufugaji wenye tija ili kuongeza thamani ya mazao yake.

Dk Mwigulu ataka tija sekta ya mifugo

Na Mwandishi
Maalumu, Dodoma

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk Mwigulu Nchemba (pichani) imeishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kusi-



**AKIKI
AJI**

na wapangaji wetu kuwa Salaam kukamilika, sasa mingine nchini. Lengo la upangaji katika nyumba

atakiwa kuwa na nyaraka

imu ya jengo (long term)

naoishi kwenye nyumba

ufanikisha zoezi hili.

O

mamia kikamilifu sekta ya mifugo kwa kubuni njia mbali mbali zita-kazooze tija katika sekta hiyo.

Dk Mwigulu ametoa ushauri huo Dodoma alipokutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa wizara hiyo ya Mifugo na Uvuvi pamoja na ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kujadili masuala mbalimbali yanayohusu namna ya kuboresha sekta ya mifugo ili iongeze mchango katika ukuaji wa uchumi wa nchi na maendeleo ya watu.

"Tutakavyoweka mipango ya kisasa ya kukuza uzalishaji katika eneo hili la mifugo, tutatengeza wigo mkubwa wa walipakodi, tutabadilisha maisha ya watu wetu, tutakuza uchumi na ajira," alisema Dk Mwigulu.

Alisema maendeleo ya sekta ya viwanda yanayokwenda kwa kasi nchini yanahitaji malighafi za kulisha viwanda hivyo na kwamba fursa zilizopo kwenye sekta ya mifugo ni kubwa na kushauri mbinu za kisasa za kuendeleza ufugaji ziwekwe bayana na kufanyiwa kazi ipasavyo.

Alisema utaratibu wa sasa wa wafugaji kuhama-hama na mifugo kutafuta malisho na maji umepitwa na wakati na kuahidi kuwa wizara yake iko tayari kutoa ushirikiano ili kufanikisha mipango ya kuendeleza sekta ya mifugo nchini.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alimshukuru Dk Mwigulu kwa kukutana nao na kuahidi kuwa ushauri uliotolewa utafanyiwa kazi kikamilifu, ambako ameunda timu ya wataalamu kwa ajili ya kuchambua mapendekezo mbali mbali yaliyotolewa katika kikao hicho alichosema kilikuwa ni cha muhimu.



"Tutaangalia namna ya kupanua na kuwa na maeneo maalum ya malisho ya mifugo yetu pamoja na kuboresha ufugaji ili ubadilike kutoka ufugaji wa kiasili kwenda ufugaji wa kisasa ili kuongeze tija," alifafanua Ndaki.

Alisema wafugaji watakaokuwa tayari kubadilisha namna ya ufugaji wao watapelekwa kwenye maeneo hayo yatakayowekewa miundombinu yote muhimu ya ufugaji ikiwemo maji, majani ya malisho na maji.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, aliishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuanzisha maeneo ya ufugaji (ranchi) kila mkoa na kujenga miundombinu itakayowasaidia wafugaji kufuga mifugo yao kisasa ili waongeze kipato chao, kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi na kuondokana na umaskini.


Naye Katibu Mkuu wa Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel aliomba Wizara ya Fedha na Mipango kujwezesha wizara yake kifedha ili kufanya utafiti katika sekta ya mifugo ili kuongeza mbinu za kisasa za kuongeza uzalishaji.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk Allan Kijazi, aliishauri kuwa ili sekta ya mifugo ipige hatua kubwa, suala la utafutaji masoko kwa ajili ya bidhaa za mifugo, kuongeza elimu kwa wafugaji, pamoja na kuwa na maeneo ya kimkakati ya viwanda vya kuchakata bidhaa za mifugo, ni muhimu likafanyiwa kazi.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Profesa Gabriel, Tanzania ni ya pili kwa kuwa na mifugo mingi Afrika ikiwa na ng'ombe milioni 33.4, mbuzi milioni 21.29, kondoo milioni 5.65, punda 657,380, lakini tija yake bado ni ndogo.

50001242

TAARIFA KWA UMMA



SILVERLANDS TANZANIA inapenda kuwataarifu wateja wetu wapendwa kuwa “**Banana Veterinary Agro Dealer**” pamoja na “**Bwana Simon Mwamvipa**” sio wasambazaji Walioidhinishwa na **Silverlands Tanzania Limited (STL)** kusambaza bidhaa yoyote ya kampuni yetu.

Hivyo basi tunapenda kuwataarifu wateja wetu kuwa hatutaweza kuunga mkono malalamiko ya mteja yeyote kuhusiana na bidhaa zinazosemekana kununuliwa kutoka kwa wafanyabiashara wasio na makubaliano na **STL**.

Ndugu wateja, kuhusiana na uhalali wa wafanyabiashara wa kilimo wanaodai kusambaza bidhaa za **STL**, tafadhali wasiliana na kituo cha usambazaji na mauzo cha **Silverlands Tanzania Limited** kilicho karibu nawe au piga simu namba **0768 119 946**.

Silverlands Tanzania Limited - chakula bora, vifaranga bora

MWANANCHI UK. 6, 07/05/2021

TALIRI livestock suitable for crossbreeding, herders told

PASTORALISTS in Dodoma and neighbouring regions have been advised to use livestock at the Tanzania Livestock Research Institute (TALIRI), Mpwapwa Centre for crossbreeding in order to obtain hybrid yields.

The call was made in Mpwapwa District by a researcher at TALIRI Mpwapwa Centre, Erick Mbisha, during a recent media tour organised by the Tanzania Commission for Science and Technology (COSTECH).

Addressing a team of journalists, Mr Mbisha said the improved cows known as Mpwapwa cattle at the centre have a capacity to grow fast and produce enough dairy and meat, adding that they are disease resistant and can survive in any Tanzania environment.

Mr Mbisha had conducted a study on breeding selection and multiplication of dairy cattle breed suitable for tropical environments.

Pastoralists need to acquire and maintain parent genetic materials from the centre and do crossbreeding, with an intention to producing an offspring that share the traits of both parent lineages, or producing an organism with hybrid vigor.

According to Mr Mbisha, at their cattle farm located at Ilo area, many pastoralists were flocking the area to buy their products and that the response from them is that they were yielding positive results.

"Many of them have been sending messages of appreciation that the Mpwapwa cattle can live in any environment and that are drought resistant," he noted.

* Nchemba wants Ministry of Livestock, Fisheries to actively manage the sector

By Guardian Reporter, Dodoma

MINISTER For Finance and Planning, Dr Mwigulu Nchemba yesterday advised the Ministry of Livestock and Fisheries, to actively manage the livestock sector by devising various ways that will increase productivity in the sector.

The minister gave the advice in Dodoma, where he met and held talks with the ministry's officials and those from the Ministry of Natural Resources and Tourism, to discuss vari-

ous issues related to how to improve the livestock sector so that it can increase the country's economic growth and human development.

"As we put in place modern programs to promote productivity in this area of livestock, we will create a large base of taxpayers, we will change the lives of our people, we will grow the economy and employment," said Dr Nchemba.

He said that the rapid development of the industrial sector in the country needs raw mate-

rials to feed industries and that the opportunities available in the livestock sector are great and advised modern methods of developing livestock should be clearly identified and implemented accordingly.

He said the current system of nomadic pastoralists in search of pasture and water was outdated and pledged that his ministry was ready to provide co-operation to facilitate plans to develop the livestock sector in the country.

For his part, the Minister

of Livestock and Fisheries Mashimba Ndaki, thanked the Minister for Finance and Planning for meeting with the leaders of the two ministries and promised that the advice given will be fully implemented where he has formed a team of experts to analyze the various proposals made in the session which he said was important.

"We will look at how to expand and have special grazing areas for our livestock as well as improve animal husbandry to change from traditional

pastoralism to modern animal husbandry to increase productivity," he explained.

He said that pastoralists who are willing to change their farming practices will be sent to the areas where all the necessary livestock infrastructure including water, pasture leaves, and water will be provided.

Permanent Secretary of the Ministry of Finance and Planning, Emmanuel Tutuba, advised the Ministry of Livestock and Fisheries to establish

ranch areas in each region and build infrastructure that will help pastoralists to modernize their livestock so that they can increase their income, contribute to the country's economic growth and eradicate poverty.

For his part, Permanent Secretary in the Ministry of Livestock and Fisheries Prof Elisante Ole-Gabriel requested the Ministry of Finance and Planning to enable its ministry financially to conduct research in the livestock sector to increase modern methods of in-

creasing productivity.

According to Prof Gabriel, Tanzania is the second largest producer of livestock in Africa with 33.4 million cattle, 21.29 million goats, 5.65 million sheep, 657,380 donkeys, but its productivity is still low.

The Permanent Secretary of the Ministry of Natural Resources and Tourism Dr Allan Kijazi, suggested that in order for the livestock sector to make significant strides, the issue of finding markets for livestock products, increasing educa-